**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

KITETE SECONDARY SCHOOL
K.S.S
MOROGORO
STRUGGLE FOR SUCCESS

Phone: 0714 907 572
0755 566 257

SHULE YA SEKONDARI KITETE,
S.L.P 662,
**MOROGORO.**

..............................

KUMB. NA. KSS/ED/JOIN/2021

JINA LA MWANAFUNZI ...............................................

...........................................................................

S.L.P ..................................................

...........................................................

**YAH: MAAGIZO KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KITETE WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021**

**1.0. UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Kitete ipo umbali wa km7, kutoka mji wa Dumila nauli Tshs. 1,000/=. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2020** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2020** ndani ya siku saba (7).

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

2.1. Sare ya shule ni suruali mbili (2) iwe na linda mbili isiwe modo rangi ya kijani kibichi (**Green forest**) na shati mbili (2) za rangi nyeupe tetron mikono mifupi na soksi jozi mbili nyeusi kwa wavulana na kwa wasichana sketi mbili (2) ivuke magoti angalau nchi nane, rangi ya kijani kibichi **(Green forest)** na shati nyeupe ya mikono mifupi na soksi nyeupe jozi mbili kwa wasichana. Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino vya kufunga. Kwa wavulana mkanda mweusi ya ngozi.

a. Rangi ya hijabu ni nyeupe inayofunika hadi tumboni.

b. Sare ya michezo kwa shule hii ni ..............................................
- Wavulana Tishirt mbili (2) rangi ya blue na track ya blue
- Wasichana Tishirt mbili (2) rangi ya blue na track ya blue.



THE HEAD MISTRESS
KITETE SEC. SCHOOL
P.O. BOX 662
MOROGORO

Scanned with CamScanner

i. Kupata mimba au kushawishi kutoa mimba
j. Kutoa mimba au kushawishi kutoa mimba
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l. Kukataa adhabu kwa makusudi
m. Kuwa na simu ya mkononi
n. Kupiga au kupigana shuleni na mitaani

4.0 **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa na mwanafunzi shuleni**.

a. Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospital ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shule.
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi /mkataba wa kutoshiriki katika migomo fujo na makosa ya jinai form hii nayo utaikabidhi kwa Mkuu wa shule.
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu **KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**.

Madamba
..............................

**MARIAM MADAMBA**
**MKUU WA SHULE**

THE HEAD MISTRESS
KITETE SEC. SCHOOL
P.O. BOX 6..
MOROGORO



Scanned with CamScanner

2.2. Daftari kumi (10 counter book) kalamu za kutosha na mkebe wa hesabu.

2.3. Chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda na kurudi pamoja na matibabu ni gharama za mzazi (mzazi mnunulie mwanao baiskeli).

**2.4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII NI:-**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu No. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria No. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais, Tamisemi, Utumishi na Utawala bora yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

**Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.**

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili na malazi na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i. Kutunza mali za Umma.

3.0. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ufukuzwe shule

a. Wizi wa aina yeyote ile
b. Uasherati, ubakaji na ushoga
c. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
d. Uvutaji sigara na bangi
e. Makosa ya jinai
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
g. Kudharau Bendera ya Taifa
h. Kuoa au kuolewa



THE HEAD MISTRESS, KITETE SEC. SCHOOL P.O. BOX 662 MOROGORO

Scanned with CamScanner

## KIAMBATANISHO A: FOMU YA KUMWANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI

OFISI YA RAIS

UTUMISHI, TAMISEMI NA UTAWALA BORA

SHULE YA SEKONDARI KITETE

(Jaza fomu hii kwa uangalifu)

Picha ya Mwanafunzi

1. Jina kamili la Mwanafunzi ____________________
2. Tarehe ya kuzaliwa ____________________ Wilaya ____________________
3. Kabila ____________________ Uraia ____________________ Dini ____________________
4. Jina la Mzazi ____________________
   Anwani ya Mzazi ____________________
   Kazi ya Mzazi ____________________ Simu na ____________________
   ____________________

(Sehemu hii ijazwe na wanafunzi ambao hawakai na wazazi wao YAANI YATIMA)

5. a. Jina la Mlezi ____________________
   b. Uhusiano kati ya Mlezi na Mwanafunzi ____________________
   c. Kazi ya Mlezi ____________________ Simu No. ____________________
   d. Anwani ya Mlezi ____________________
   ____________________
6. Shule atokayo mwanafunzi ____________________
7. Wakati wa likizo mwanafunzi atakwenda wapi? ____________________
8. Maelezo ya mwanafunzi ____________________
   ____________________
9. Ujuzi (Stadi) mwingine ____________________
10. Saini ya mwanafunzi ____________________
    ____________________



THE HEAD MISTRESS
KITETE SEC. SCHOOL
P.O. BOX ...
MOROGORO

Scanned with CamScanner

KIAMBATANISHO B: FOMU YA KUMWANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI

OFISI YA RAIS
UTUMISHI, TAMISEMI NA UTAWALA BORA
SHULE YA SEKONDARI KITETE

Mimi ________________________________________ Msichana /Mvulana
Ninakubali kuingia kidato cha __________________ katika shule ya Sekondari KITETE.

Kama mwanafunzi wa kutwa tarehe _______________ nitafika shuleni bila kuchelewa.

Nitatii sheria za shule na nitaishi maisha mazuri. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea, nitalazimika kulipa uharibifu wowote uwe ni majengo, vitabu na vitu vyote nitakavyoharibu nikiwa shuleni.
Sahihi ya mwanafunzi ____________________ tarehe _________________

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI:** Mimi ________________________________ ninakubali mtoto wangu ____________________________________ asome katika shule ya sekondari Kitete kuanzia tarehe __________________________
Ninahaidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua.

Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.

Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubaliwa kuingia katika shule ya Sekondari KITETE kama mwanafunzi wa kutwa. Hivyo muda wa mwanafunzi kuwa shuleni ni saa 1 asubuhi hadi saa 9 mchana, na nitawajibika kwa malezi ya ziada kwa muda ambao si wa masomo na siku za mapumziko.

Anwani yangu ya kudumu ni:-

________________________________________________________________________

____________________________________

Sahihi _____________________________ tarehe _________________



THE HEAD MISTRESS
KITETE SEC. SCHOOL
P.O. BOX 652
MOROGORO

## APPENDEX C: MEDICAL EXAMINATION FORM

KITETE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 662,
MOROGORO.

Date __________/20 ________

PART A:

Mr./Miss ______________________________________________

Please examine the above named student as to his/her physical and mental Fitness for full time student in this school. The examination should include the following categories:-

1. Haemoglobin ______________________
2. P.V bleeding ______________________
3. Sight ______________________
4. Blood pressure ______________________
5. Urine for sugar ______________________
6. Stool for routine examination ______________________
7. Pregnancy test ______________________
8. Skin diseases ______________________
9. Leprosy ______________________
10. Any deformity ______________________
11. Epilepsy ______________________
12. Pulmonary tuberculosis ______________________
13. Neurosis ______________________
14. Venereal diseases ______________________
15. Other serious diseases ______________________

PART B.

(To be completed by a Government Medical Officer)

1. I have examined the above named student and consider that he/she is Physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time schooling.
2. Other Comments ______________________________________________
______________________________________________
3. Date ______________________ Signature ______________________
Station ______________________ Designation ______________________
Official stamp ______________________



THE HEAD... KITETE ... SCHOOL P.O. ... 662 MOROGORO

Scanned with CamScanner